

Kuzuia Wizi wa Dukani

Wizi wa dukani hugharimu biashara makumi ya mabilioni ya dola kila mwaka. Kiwango cha wastani cha upotevu ni 1.33% (Chanzo: Utafiti wa Shirikisho la Taifa la Wauzaji Rejareja). Biashara za kila aina zinakabiliwa na uwezekano wa wizi wa rejareja. Kutumia huduma bora kwa wateja, pamoja na teknolojia na sera na utaratibu madhubuti kunaweza kupunguza hatari zinazozikabili biashara.

Usanifu ni Muhimu (Kuzuia Uharifu kupitia Usanifu wa Mazingira)

- **Upelelezi wa Asili** – Wafanyakazi na wateja lazima wawewe kuona na kipeleleza vizuri eneo hiyo.
 - Hakikisha kuna mwangaza wa kutosha ndani na nje.
 - Weka mpangilio wa chini ili kuhakikisha sehemu za sakafu zinaonekana vizuri.
 - Ondo Vitu Visivyo Muhimu
- **Kumiliki Eneo** – Dai sehemu, fafanua madhumuni yake na uonyeshe umiliki.
 - Alama zinazonekana vizuri zinazofafanua maeneo ya wateja na wafanyakazi.
- **Udhibiti wa Kuingia** – Uwekaji wa vizuizi ili kuongeza utambuzi wa hatari kwa mhalifu.
 - Idadi ndogo ya milango ya kuingilia/kutokea.
 - Bohari na ofisi zilizofungwa.
- **Utunzwaji** – Sehemu iliyotunzwa vizuri huonyesha ufuatiliaji na hupunguza watumiaji haramu na/au wasumbufu.
 - Hakikisha sakafu ya mauzo na vyumba vya kujaribishia nguo ni safi na viko katika mpangilio mzuri.

Mambo ya Msingi

- Tekeleza huduma bora kwa wateja – msalimie kila mtu anayeingia; wasiliana tena na wateja ili kuwapa huduma.
- Dumisha usafi na mpangilio mzuri katika eneo hiyo.
- Kagua na usafishe vyumba vya kujaribia nguo mara kwa mara.
- Tangaza sera zako za kupinga wizi.
- Hakikisha mabohari na ofisi zimefungwa zinapokuwa hazitumiki.
- Weka sehemu ya kulipia katika eneo linaloonekana vizuri karibu na mlango.
- Weka vioo mbonyeo kimkakati ili kuwezesha eneo kubwa la biashara lioneokane vizuri.

Hamia katika Teknolijia

- Funga kamera zenye ubora wa hali ya juu ili kuhakikisha kuwa picha bora zaidi zinapigwa – hakikisha zinarekodi mlango wa kuingilia/kutokea, sehemu ya mauzo, bohari, maeneo yoyote ya kupokelea na kushughulikia pesa.
- Tumia upelelezi wa alama za kielektroniki au mifumo ya RFID kwenye bidhaa.
- Tumia njia salama ya kushuka ambayo imefungwa kwenye sakafu.
- Weka alama zinazoonesha kuwa kiasi kidogo cha pesa kiko kwenye majengo.
- Dhibiti urejeshaji bidhaa na urejeshaji wa pesa ili kuzuia udanganyifu.

Nyenko

Idara ya Polisi ya Albuquerque, Timu ya Kuzuia Uhalifu inaweza Kuzuia Uhalifu kupitia utafiti wa Usanifu wa Mazingira (CPTED). Pia, Kitengo cha Kuzuia Uhalifu kinaweza kutoa msaada wa mahitaji yako ya mafunzo kuhusu mada hii na zingine.

Shirikisho la Taifa la Wauzaji Rejareja: <https://nrf.com/>

Chama cha Wataalamu wa Sekta ya Kuzuia Upotevu: <http://www.ipipagroup.com/>



ONE
ALBUQUE
RQUE
APD